COLORADO
Department of
Labor and Employment

Bango la Haki za Ustawi wa Umma na Eneo la Kazi la Colorado:
Likizo ya Malipo, Uanikaji Masuala, & Kifaa Binafsi cha Kujilinda

Idara ya Viwango & Takwimu za Ajira

Linalotekelezeka Kwanzia Julai 15 - Desemba. 31, 2020

SHERIA YA USTAWI WA FAMILIA & MAENEO SALAMA YA KAZI ("HFWA"):
Haki ya Muajiriwa Kupewa Likizo ya Malipo

Waajiri waliopo Colorado Wanapaswa Kutoa Likizo ya Malipo kwa ajili ya Mahitaji ya COVID-19 Hadi Kufika Desemba 31, 2020

- Waajiri waliopo Colorado wanapaswa kutoa likizo ya malipo katika mwaka wa 2020 kwa muajiriwa ambaye:
  (1) ana **dalili za COVID-19** na anatafuta kupata utambuzi wa kimatibabu;
  (2) ameelekezwa na wakala wa serikali ama mtoaji huduma ya afya **kukaa kwenye karantini ama kujitenga** kutokana na hatari ya COVID-19; ama
  (3) **anayemhudumia mtu mwingine** kutokana na tahadhari za COVID-19 – iwe ni mtu aliyeamrishwa kujiweka kwenye karantini ama kujitenga, au mtoto ambaye shule yake, ama sehemu ya malezi au kituo cha watoto kimefungwa au kutopatikana.
- Kwanzia 2021, HFWA itahitaji kuwepo kwa likizo yenye malipo yaliyopunguzwa (lisaa 1 kwa masaa 30 yaliyofanyiwa kazi, huku kiasi cha juu zaidi kikiwa masaa 48 ya likizo yenye malipo kwa mwaka) hata hivyo itajumuisha wigo mpana wa masharti, na itaongezea masaa ya nyongeza 32 katika likizo ya malipo (jumla 80) katika huduma za dharura ya kiafya kwa umma.

Kiasi gani cha likizo ya Malipo: Hadi Wiki Mbili (Masaa 80)

- Waajiriwa wanaweza kuchukua **hadi wiki 2** za likizo ya malipo: **hadi masaa 80**, kutegemeana na masaa yao ya kila wiki.
- Likizo ya malipo itakuwa ndani ya **kiwango cha kawaida cha malipo** cha muajiriwa, ama kinaweza kuwa katika **⅔ ya malipo kwa kikundi cha #3** (kumhudumia mtu mwingine). Kiwango hiki cha malipo hakitajumuisha malipo ya muda wa ziada wa kazi wala bonasi. Ikiwa malipo yatategemeana na mauzo kiukamilifu ama kwa sehemu, basi likizo ya malipo itapaswa kuwa kwa mujibu wa kiwango cha muajiri cha malipo ya lisaa ama mshahara, ama kiwango cha chini cha ujira kinachotumika (chochote kitakachokuwa cha juu zaidi).
- Ikiwa muajiriwa atakuwa amekwishapokea likizo ya malipo ndani ya 2020 kwa ajili ya mahitaji yanayohusiana na COVID-19, likizo hiyo itajumuishwa kuwa sehemu ya wiki 2 ambazo HFWA inahitaji, hata hivyo likizo iliyotolewa kwa madhumuni *yasiyo*husiana na COVID haitohesabika kuwa sehemu ya kile HFWA inachokihitaji.

Malipizi ama Uingilizi wa Haki za HFWA

- Muajiri hawezi kumfuta kazi, kumpatia vitisho, ama **kulipiza kisasi dhidi ama kuingiliana na**, muajiriwa ambaye: (A) ameomba ama amechukua likizo ya HFWA; (B) amemuarifu mtu mwingine kuhusiana na haki za HFWA, ama ameunga mkono kuwa mtu aweze kutekeleza haki zake za HFWA; (C) amefungua malalamiko ya HFWA; ama (D) ameshirikiana/kusaidia katika uchunguzi unaohusiana na ukiukwaji wa HFWA.

  •Ikiwa lalamiko la HFWA la muajiriwa, ombi, au shughuli nyingine yoyote itakuwa *si sahihi*, muajiri hatohitajika kulikubali ama kulitekeleza – hata hivyo bado hatoweza kumfukuza kazi ama kuchukua *hatua dhidi ya* muajiriwa huyo kutokana na hilo, almradi kuwa imani ya muajiriwa ilikuwa yenye mantiki na katika nia nzuri. Waajiriwa *wanaweza* kukumbana na matokeo ya kutumia vibaya likizo ya malipo ama mwenendo mwingine usiofaa.

Hujumuisha: Waajiri na Waajiriwa Wote, isipokuwa kwa maeneo machache

- **Waajiri wote waliopo Colorado**, **bila kujali ukubwa wao**, watapaswa kutoa likizo ya malipo ya HFWA, isipokuwa tu kwa maeneo ya serikali ya jumuisho (waajiriwa wengine wa serikali watahusika) na wale wanaofunikwa na Sheria ya Serikali ya Jumuisho ya Bima ya Ukosefu wa Ajira ya Reli.

  •Waajiri wenye **pungufu ya waajiriwa 16 hujumuishwa katika mwaka wa 2020, hata hivyo wataondolewa kwenye mwaka wa 2021 (kisha waajiri wote watajumuishwa kwenye mwaka wa 2022)**

  •Waajiri wanaotoa likizo ya malipo "inayolingana nayo au kuzidi" kupitia makubaliano yaliyojadilika kwa pamoja hawajajumuishwa kwenye matakwa ya HFWA, almradi tu wasiondoshe haki kama vile haki dhidi ya malipizi ama haki ya kufungua malalamiko.
- Makubaliano ya muajiriwa ama sera za muajiri **haziwezi kuondosha haki za HFWA**, na ni zenye utupu na zisizoweza kushurutishika kisheria.

SHERIA YA UANIKAJI WA DHARURA YA KIAFYA KWA UMMA ("PHEW"):
Haki za Wafanyakazi za Kueleza Juu ya Masuala ya Kiafya Kazini & Matumizi ya Vifaa vya Kujikinga

Haki za Wafanyakazi za Kupinga Ukiukwaji wa Kiafya/Usalama Kazini katika Vipindi vya Dharura za Kiafya kwa Umma

- Ni kinyume cha sheria kupinga, kuingilia, shughuli zifuatazo katika kipindi, ama kile kinachohusiana na, dharura ya kiafya kwa umma:
  (1) **utoaji wasiwasi wenye mantiki**, iwe ni lalamiko rasmi ama lisilo rasmi kwa mtu yoyote, kuhusiana na ukiukwaji wa kanuni za afya ama usalama za serikali, ama kuhusiana na tishio la afya ama usalama lenye uzito katika sehemu ya kazi;
  (2) **kupinga** ukiukwaji (wa aina ya kundi la 1); ama
  (3) **kushuhudia, kusaidia, ama kushiriki** katika shughuli ya kimahakama inayohusiana na ukiukwaji (wa aina ya kundi la 1).

• Ikiwa lalamiko la PHEW la muajiriwa, ombi, au shughuli nyingine yoyote itakuwa *si sahihi*, muajiri ama biashara nyingine haitohitajika kulikubali ama kulitekeleza – hata hivyo bado hatoweza kumfukuza kazi ama kuchukua *hatua dhidi ya* muajiriwa huyo kutokana na hilo, almradi kuwa imani ya muajiriwa ilikuwa yenye mantiki na katika nia nzuri. Waajiriwa *wanaweza* kukumbana na matokeo ya kutumia vibaya haki za PHEW ama mwenendo mwingine usiofaa.

Haki za Wafanyakazi za Kutumia Vifaa vyao Binafsi vya Kujikinga ("PPE")

- Mfanyakazi anapaswa kuruhusiwa **kwa hiari yake kuvaa Vifaa vyake Binafsi vya Kujikinga (PPE)**, kama vile barakoa, kifunika uso, ama glovu, ikiwa PPE hiyo:
  (1) itatoa **ulinzi zaidi** kuliko kifaa kinachotolewa kazini;
  (2) **imependekezwa** na wakala wa afya wa serikali (serikali ya jumuisho, chi, ama manispaa);
  (3) haimfanyi mfanyakazi huyo **kushindwa kufanya kazi**.

Hujumuisha: Waajiri na Waajiriwa Wote, Pamoja na Wakandarasi Binafsi Kadhaa

- PHEW hutumia maneno "**mkuu**" na "**mfanyakazi**" (si muajiri/muajiriwa) kwa sababu hayo hujumuisha wakandarasi binafsi.
  (1) Muajiri yoyote aliyepo Colorado, *na* biashara yoyote iliyopo Colorado yenye wakandarasi binafsi *5 au zaidi*, itawekwa katika "mkuu" ambaye atapaswa kufuatana na PHEW. Serikali ya jumuisho haijaingizwa ndani ya sheria hii.
  (2) Muajiriwa yoyote *ama* mkandarasi aliyeingizwa kwenye "mkuu" ni "mfanyakazi" aliyejumuishwa katika PHEW.

HAKI YA MALALAMIKO (chini ya HFWA & PHEW)

- Shutuma za ukiukwaji zinaweza kuwasilishwa katika Idara kwa ajili ya uchunguzi (taarifa za mawasiliano zipo hapa chini).
- **Kushindwa kutoa likizo ya malipo** chini ya HFWA ni dai la "ujira ambao haujalipwa" ambalo Idara **itapaswa** kuchunguza na kuamua.
- **Malipizi ama Uingilizi** wa haki za PHEW ama HFWA ni dai ambalo Idara **inaweza** kuchunguza kisheria. Idara hii itatathmini madai kama hayo yote, na kama uamuzi utakuwa ni **kutokufanya** uchunguzi, Idara hii itamtaarifu mdai.
- Shutuma za ukiukwaji zinaweza kwa njia mbadala kufunguliwa mashtaka mahakamani, lakini ni baada tu ya suluhisho hizi zisizo za mashataka ya kisheria kufanyika.
- **HFWA**: shitaka la kisheria (A) haliwezi kufunguliwa *mpaka* pale muajiri atakapopewa mswada wa kimaandishi na siku 14 za kutoa majibu, na (B) haliwezi kufunguliwa *ikiwa* Idara itachunguza na kuamua dai hilo (ambalo pande hizo wanaweza kukata rufaa).
- **PHEW**: shitaka la kimahakama haliwezi kufunguliwa bila kwanza kufungua dai kwenye Idara, kisha (A) *linaweza* kufunguliwa ikiwa Idara *haito* peleleza, na (B) *haliwezi* kufunguliwa ikiwa Idara itachunguza na *kuamua* dai hilo (ambalo pande hizo zinaweza kukata rufaa).

Bango hili linaeleza kwa ufupi sheria za ustawi wa umma na eneo la kazi za Colorado, SB 20-205 (likizo ya malipo) na HB 20-1415 (uanikaji masuala na kifaa binafsi cha kujikinga). Halijumuishi sheria nyingine za afya ama usalama, kanuni, na oda, zilizopo chini ya Sheria ya Sheria ya Usalama na Ustawi Mahali pa Kazi (OSHA), kutoka Idara ya Colorado ya Ustawi na Mazingira ya Umma (CDPHE), ama kutoka wakala za manispaa za ustawi wa jamii. Wasiliana na vyombo hivyo ili kupata taarifa zaidi zinazohusiana na ustawi na usalama wa umma.

Bango hili sharti liwekwe sehemu ambapo linaweza kufikika na wafanyakazi, kushirikishwa kwa wafanyakazi wa mbali kieletroniki ama kwenye karatasi, na kuchukuliwa nafasi na bango la 2021 ifikapo Januari 1, 2021.

Kwa taarifa zaidi, ama kama tafsiri za lugha nyingine zitahitajika, wasiliana na: Idara ya Viwango & Takwimu za Ajira, coloradolaborlaw.gov, cdle_labor_standards@state.co.us, 303-318-8441 / 888-390-7936.